# Uchanganuzi wa Vigezo Vinavyotumika Kuwajenga Wahusika katika Ushairi wa Kiswahili

*Baraka Sikuomba* na *Joviet Bulaya*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

**Ikisiri**

**Makala hii imechunguza vigezo vilivyotumiwa kuwajenga wahusika katika ushairi wa Kiswahili. Makala hii imetokana na madai ya tafiti kueleza kwamba mashairi mengi andishi hayana wahusika bali mashairi simulizi (Samwel, Selemani na Kabiero; 2013). Kutokana na madai hayo tuliona ipo haja kuchunguza vigezo vinavyotumika kuwajenga wahusika katika ushairi andishi wa Kiswahili pamoja na wahusika waliojengwa kupitia vigezo hivyo. Ili kutimiza azma ya makala hii, utafiti umefanywa kwa kurejelea diwani tatu, yaani *Fungate ya Uhuru* (1988), *Wasakatonge* (2003) na *Vifaru Weusi* (2016). Data za msingi za makala hii zilipatikana maktabani kwa mbinu ya usomaji matini na uchambuzi wa nyaraka. Kadhalika, katika makala hii Nadharia ya Uhalisia ndiyo iliyoongoza mchakato mzima wa uwasilishaji na uchambuzi wa data. Matokeo ya utafiti yaliyozaa makala hii yameonesha vigezo kama vile kigezo cha kitaswira, kigezo cha usimulizi, kigezo cha kifasihi simulizi na kigezo cha kiishara ndivyo vilivyotumiwa na mwandishi Seif Khatib kuwajenga wahusika katika diwani teule. Pia, makala hii imeonesha kila kigezo kilivyotumika kuwajenga wahusika katika ushairi wa Kiswahili kupitia diwani teule za makala hii. Makala hii inapendekeza kufanyika kwa tafiti nyingine katika fasihi andishi zitakazotofautisha na kulinganisha vigezo vinavyotumika kuwajenga wahusika wa ushairi na tanzu nyingine za fasihi andishi kama vile riwaya, tamthiliya na hadithi fupi.**

**Neno Muhimu:** *Wahusika*

**Utangulizi na Mapitio ya Maandishi**

Suala la wahusika katika kazi za kifasihi limejadiliwa kwa namna mbalimbali. Mathalani, katika ushairi wa Kiswahili, Samba (2018) anaeleza kuwa ni vigumu kuwatambua wahusika katika ushairi wa Kiswahili kutokana na muundo wa utanzu husika. Kwa upande mwingine, M'Ngaruthi (2019) katika utafiti wake uliohusu usawiri wa wahusika katika mashairi ya Mbega (1984) na yale ya Mohamed (2002) anakiri kuwapo kwa wahusika kama vile binadamu, wahusika wanyama, vitu visivyo hai na viungo vya mwili katika ushairi wa Kiswahili. Wahusika hao hupatikana na kudhihirika katika mazingira ya kijiografia, kihistoria, kiuchumi na kisiasa. Pamoja na tafiti za wataalamu tuliowapitia awali kuzungumzia masuala ya wahusika katika ushairi wa Kiswahili bado haiko bayana ni vigezo gani hasa vilivyotumiwa na mwandishi wa diwani teule za makala hii kuwajenga wahusika. Hii inatokana na uwapo wa wahusika wanaosawiri jamii na mabadiliko yake katika diwani teule waliosawiriwa kutokana na muundo legezo alioutumia mwandishi Muhammed Seif Khatib katika diwani ya *Fungate ya Uhuru* (1988), *Wasakatonge* (2003) pamoja na *Vifaru Weusi* (2016).

Uchambuzi wa vigezo vilivyotumiwa kuwajenga wahusika katika diwani teule umezingatia Nadharia ya Uhalisia. Nadharia hii hurejelea mtindo wa uandishi unaomakinika na utoaji wa picha halisi ya maisha ya kawaida katika jamii mahususi (Dargan, 1932). Nadharia hii iliasisiwa katika karne ya kumi na tisa na kufafanuliwa zaidi na Goffman (1952). Nadharia ya Uhalisia pia hutoa taswira au picha halisi ya maisha ya kawaida ya watu katika jamii mahususi na inajihusisha na utanzu wa fasihi andishi (Mbatiah, 2016). Kwa mantiki hiyo, uhalisia unamwona binadamu kama zao la ulimwengu ambao unamfinyanga ili aonekane jinsi anavyoonekana katika jamii (Marques, 2009). Katika mawanda ya fasihi, uhalisia wa matatizo yaliyokuwa yakiwakabili watu uliwafanya wanasanaa kuushutumu ulimbwende kwani matamanio yao yalikuwa ya kinjozi zaidi ukilinganisha na taabu zilizokuwa zinawakabili watu (Gouldin, 1961).

Kihistoria, Nadharia ya Uhalisia ilitumiwa kwa mara ya kwanza katika fasihi kule Ufaransa mnamo mwaka 1850 kwa lengo la kufafanua kazi za sanaa zilizojikita katika kusawiri ulimwengu kama ulivyo (Qusby, 1988). Naye Ruan (1986) anadai kuwa matumizi kamili ya Nadharia ya Uhalisia katika fasihi yalianza kuonekana katika katika kazi ya Erich Auerbach ya 1948 iliyojulikana kama *Mimesis*. Miongoni mwa waasisi wake ni Gustave Flaubert ambaye alikuwa na dhana kwamba mtu hufikiria kwa kichwa chake si kwa moyo wake. Wafula na Njogu (2007) wanafafanua zaidi kwamba dhana ya Gustave ilisisitiza umuhimu wa kueleza na kubainisha matatizo ya kijamii katika uhalisi na uyakinifu wake. Utunzi wa kazi zisizo za kiuhalisia ulichochea kuibuka kwa Nadharia ya Uhalisia ambayo ilitumiwa kwa mara ya kwanza katika fasihi na mwandishi maarufu wa riwaya nchini Ufaransa aliyefahamika kwa jina la Jules Husson Champfley kwa kuwachora wahusika wake kulingana na mazingira halisi ya jamii (Gouldin, 1961). Makala hii imeongozwa na msingi wa Nadharia ya Uhalisia uliowekwa na Hegel (1979) unaoeleza kuwa mwandishi huchagua wahusika ambao ni vielelezo na mifano ya watu wanaoishi katika jamii. Hivyo basi, Nadhaaria ya Uhalisia imetusaidia kubaini vigezo vilivyotumika kuwajenga wahusika katika diwani teule.

**Methodolojia**

Data iliyotumika katika makala hii ilikusanywa kwa njia ya usomaji makini wa matini na uchambuzi wa nyaraka katika diwani za *Fungate ya Uhuru* (1988), *Wasakatonge* (2003) na *Vifaru Weusi* (2016). Katika diwani hizi, vigezo mbalimbali vilivyotumika kuwajenga wahusika vilikusanywa. Vigezo vya kuwajenga wahusika vilikusanywa kulingana na mtindo wa wahusika uliotumiwa na mwandishi katika kila diwani. Kwa kuzingatia aina ya wahusika, vigezo vilitambuliwa kwa sababu ya wahusika waliotumiwa na mwandishi kujengwa kisanaa kwa kuchotwa kwa sehemu kubwa katika mashairi simulizi. Pia, data ilichanganuliwa kutoka katika mashairi kumi na mawili ambapo manne ni kutoka katika diwani ya *Fungate ya Uhuru*, manne kutoka katika diwani ya *Wasakatonge* na manne kutoka katika diwani ya *Vifaru Weusi* kwa kuzingatia msingi wa Nadharia ya Uhalisia.

**Matokeo ya Utafiti**

Matokeo ya utafiti huu yamechambuliwa katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza imechambua vigezo vilivyotumika kuwajenga wahusika katika diwani teule na sehemu ya pili ni wahusika waliojengwa kulingana na kila kigezo.

**Kigezo cha Kitaswira**

Taswira ni picha ambayo humjia mtu akilini anaposoma, kutazama au kusikiliza kazi ya fasihi (Ogutu, 2021). Aidha, Ogutu anafafanua kuwa taswira huweza kufumbata maana fiche za kijazanda. Hii ina maana kwamba, wahusika wa kitaswira hutumiwa kuwasilisha ujumbe au wahusika halisi kwa namna ambayo si ya wazi. Kwa upande wa diwani teule za utafiti huu, Uchambuzi wa data umebaini kuwa, baadhi ya taswira zilizotumiwa na mwandishi wa diwani teule zimewasilisha wahusika mbalimbali. Aidha, Waititu na Oyugi (2005) wanaeleza kuwa taswira ni mbinu ambayo msanii hutumia maneno yanayotoa picha halisi ya yale anayojaribu kueleza kiasi cha kumfanya msomaji kupata picha iliyokusudiwa akilini na mawazoni mwake. Kwa hiyo, katika diwani teule, kigezo cha kitaswira kimewajenga wahusika wa kitaswira kama watu waliotumiwa na msanii kuonesha hali halisi ya uhusiano wa kiutabaka na kinyonyaji unavyolitesa tabaka la chini licha ya kazi ngumu wanazozifanya katika jamii. Uchambuzi na uwasilishaji wa wahusika wa kitaswira umefafanuliwa katika vipengele vifuatavyo:

**Wahusika Wasakatonge**

Utafiti huu umebaini kuwa katika diwani ya *Wasakatonge* (2003) mwandishi ametumia kigezo cha taswira kuwajenga wahusika wasakatonge ambao wanawakilisha tabaka la chini. Kama ilivyoelezwa na Sengo (1993) matabaka hurejelea mgawanyiko wa jamii unaotokana na kubaguana kwa misingi ya dini, kipato, kikabila, kielimu, kijinsia au kazi aliyonayo mtu. Katika diwani ya *Wasakatonge* mwandishi ametumia taswira ya wasakatonge kuonesha uhusiano wa kitabaka baina ya viongozi wa

nchi na wananchi wao. Aidha, licha ya wasakatonge kufanya kazi za jasho bado maisha yao yamebaki kuwa duni. Katika shairi la 'Wasakatonge' mwandishi anasema:

(1)

**Wasakatonge**

5 *Wasakatonge* na juakali
**Wabeba zege** ya maroshani,
Ni msukuma mikokoteni,
Pia makuli bandarini,
Ni wachimbaji wa migodini,
Lakini maisha yao chini.

6 Juakali na **wasakatonge,**
Wao ni manamba mashambani,
Ni wachapa kazi viwandani,
Mayaya na madobi wa nyumbani,
Ni matopasi wa majaani,
Lakini bado ni masikini.

3 Wao huweka serikalini,
Wanasiasa madarakani,
Dola ikawa mikononi,
Wachaguliwa wa ikuluni,
Lakini wachaguaji duni.

4 **Wasakatonge** na juakali,
Wao ni wengi ulimwenguni,
Tabaka lisilo ahueni,
Siku zote wako matesoni,
Ziada ya pato hawaoni,
Lakini watakomboka lini?

**Chanzo:** Diwani ya *Wasakatonge* (uk. 5)

Katika dondoo hilo imebainika kuwa taswira ya wasakatonge imewakilisha watu wa tabaka la chini. Tabaka hili limebainishwa kulingana na kazi zao kama vile; kubeba zege, kusukuma mikokoteni, ukuli bandarini, uchimbaji madini migodini, manamba wa mashambani, mayaya na madobi wa nyumbani, pamoja na utopasi. Kazi zote hizi ni kazi zinazohitaji nguvu na zinafanywa na watu wa tabaka la chini kwa lengo la kujikwamua na umaskini. Hata hivyo, hali huwa tofauti kutokana na tabaka la juu linaloongozwa na wanasiasa kuendeleza unyonyaji katika mapato dhidi ya tabaka tawaliwa. Data hiyo, inaelekeana na mawazo ya Hussein (1988) anayeeleza kuwa matabaka ni chanzo cha matatizo mengi katika jamii kutokana na watu kukosa huduma za msingi kutokana na kipato kidogo walichonacho. Kwa mfano, dondoo hiyo limeonesha kwamba tabaka la chini ndilo lenye mamlaka ya kuwaingiza viongozi wa kisiasa ikuluni kwa njia ya kura. Lengo kuu la kufanya hivyo ni kuhakikisha viongozi hao wanashughulikia matatizo ya wapiga kura wao. Nadharia ya Uhalisia imetuongoza kubaini kuwa mambo huwa tofauti kutokana na sababu kwamba, viongozi wa kisiasa wakishachaguliwa huishia kujinufaisha ikuluni na kulifanya tabaka la chini lililowapigia kura kukosa mtetezi. Hali hii imewafanya watu wa tabaka la chini kuishi maisha ya kimaskini na kushindwa hata kujiwekea akiba katika mapato wanayoyapata kutokana na unyonyaji unaofanywa dhidi yao na tabaka tawala.

**Wahusika Vifaru Weusi**

Katika diwani ya *Vifaru Weusi* (2016) mwandishi ametumia taswira ya Vifaru Weusi kuwakilisha viongozi wa Afrika jinsi wanavyotumia madaraka yao kimabavu bila kufuata demokrasia. Aidha, ili kuweza kufikia matakwa yao, viongozi wa Kiafrika wanatumia nguvu na mabavu kama silaha yao ya kuwadhoofisha na kuogofya watu katika mabara yao. Hili limebainishwa na msanii kupitia shairi la 'Vifaru Weusi' kama mwandishi anavyosema:

(2)

**Vifaru Weusi**

**Vifaru weusi**,
Wanaranda na kutamba,
Wanatumia mabavu,
Kwa mabavu,
Na pia kwa maguvu,
Na kugofisha,
Ili kudhoofisha,
Ndani ya nyika,
Kwetu Afrika,
Hakukaliki,
Ni mateso.
Vinyama vidogo,
Viswala na digidigi
Si ngiri wala si fisi,
Hawana nafasi
Wote wanateswa.
Na wananyanyaswa,
Na kudhalilishwa,
Ndani ya nyika,
Kwetu Afrika
Hakuishiki.

**Chanzo:** Diwani ya *Vifaru Weusi* (uk. 1)

Kupitia dondoo hii, tumebaini kuwa Vifaru Weusi wamechorwa kitaswira na mwaandishi ili kuakisi uhalisia wa viongozi tulionao katika bara la Afrika. Katika dondoo hilo imebainika kuwapo kwa matabaka mawili yaani tabaka la chini na tabaka la juu. Aidha, kwa kuongozwa na msingi wa Nadharia ya Uhalisia unaodai kuwa mwandishi huchagua wahusika ambao ni vielelezo na mifano ya watu wanaoishi katika jamii, utafiti huu umebaini kuwa tabaka la juu limewasilishwa na Vifaru Weusi wanaotumia mabavu na maguvu wakati tabaka la chini linalowakilishwa na viswala, digidigi ni ambalo linateswa na kunyanyaswa katika nchi yao hususani Afrika. Manyanyaso kama vile, kuteswa, kunyanyaswa na kudhalilishwa wanayokutana nayo tabaka la chini ndani ya nchi zao hususani Afrika, yanazifanya nchi nyingi za Afrika kukosa utulivu. Hali hii imesababisha nchi nyingi za Afrika kushindwa kukalika kutokana na migogoro inayosababishwa na uonevu pamoja na utawala wa kimabavu unaofanywa na viongozi wengi katika nchi hizo dhidi ya tabaka tawaliwa.

**Kigezo cha Uhalisia wa Wahusika**

Kulingana na Chomba na Kakivi (2018) wahusika halisi ni wahusika ambao hutumiwa kinyume na wahusika wanyama kwa mantiki kwamba uhalisia wao hudhihirika kupitia majina yao ambayo ni ya majazi au kinaya. Kadhalika, Chombo na Kakivi wanaeleza kuwa wahusika huelezwa kama wa kihalisia ikiwa watafanana na sura fulani ya maisha katika jamii. Katika diwani ya *Wasakatonge* (2003), mwandishi ametumia kigezo cha wahusika halisi mbalimbali ambao wamewakilisha hali halisi iliyomo katika jamii. Hili limebainishwa kupitia wahusika wakulima na wafanyakazi kama ifuatavyo:

**Wahusika Wafanyakazi na Wakulima**

Makala hii imebaini kuwa kigezo cha uhalisia wa wahusika kimetumiwa na mwandishi wa diwani teule za Makala hii kuwakilisha wahusika wafanyakazi na wakulima. Mlacha (1985) anashadidia hoja hii kwa kueleza kuwa wafanyakazi na wakulima ni wahusika wa kihalisia wanaotumika katika kazi za fasihi kuwakilisha makundi ya kitabaka katika jamii. Aidha, data za makala hii zimeonesha kwamba, makundi haya mawili ya wahusika yaani wakulima na wafanyakazi wanapaswa kuungana ili waweze kufanikiwa katika mapambano dhidi ya tabaka tawala. Katika diwani ya *Fungate ya Uhuru* (1988) kupitia shairi la 'Unganeni" mwandishi amelieleza hili anaposema:

(3)

**Unganeni**

**Wafanyakazi** wa Afrika, tuunganeni,
Na **wakulima** kadhalika, tushikaneni
Makabwela mnaosumbuka, tukutaneni
Tujiandae kwa Mapambano, yalo marefu
  Ushindi ni wetu
Msimamo wa kitabaka, tuwekeni,
Bepari wote kuwashika, wawe ndani,
Na mamwinyi bila shaka, wambaroni,
Tusizubae, kazi ianze, twangoja nini?
  Wakati ni huu.
Itikadi ya mapinduzi, ni sukani,
Nayo tuifanyie kazi, vitendoni,
Kwa wanafiki viongozi, tutumieni,
Tusiajizi, kwa mdhalimu, wanaodhulumu
  Harakati tuanze.

**Chanzo:** Diwani ya *Fungate ya Uhuru* (uk. 1)

Dondoo hii linaonesha jinsi wakulima na wafanyakazi wanavyopaswa kuwa na umoja katika mapambano dhidi ya umasikini. Ili umoja kati ya wakulima na wafanyakazi uwepo, imebainika kuwa wanapaswa kuungana, kushikamana, kukutana, kuwa na mapambano ya muda mrefu ya matabaka, kutozubaa na kuanza itikadi za mapinduzi dhidi ya mabepari na mamwinyi. Aidha, ili kuweza kufanikisha itikadi ya mapinduzi ni lazima kukomesha viongozi wanafiki na wadhalimu wanaodhulumu haki za wafanyakazi na wakulima kuwa wamoja. Vilevile, msingi wa Nadharia ya Uhalisia unaodai kuwa mwandishi huchagua wahusika ambao ni vielelezo na mifano ya watu wanaoishi katika jamii umetuongoza kubaini kuwa suala la utabaka linapaswa kuachwa ili kuwabaini mabepari na mamwinyi kama ajenda ya mapinduzi na kuwatokomeza viongozi wanafiki, wadhalimu na wanaodhulumu. Data hii imeendana na hoja ya Bosibori (2016) anayaeeleza kuwa wafanyakazi wengi na wakulima hawawezi kumudu mahitaji yao ya msingi kama vile chakula, mavazi, matibabu na elimu. Ili kukomesha hali hii wanapaswa kuwa wamoja. Hivyo, matokeo ya uchunguzi wetu yameonesha kwamba njia pekee ya wafanyakazi na wakulima kujikomboa ni kuungana na kuwa na itikadi za kimapinduzi dhidi ya tabaka tawala linalowanyonya kimaslahi.

**Kigezo cha Kisiasa**

Halikadhalika, katika diwani teule imebainika kuwa kigezo cha kisiasa kimetumika kuwajenga wahusika wa kisiasa. Masaku (2018) anaeleza kuwa siasa ni mfumo mahususi wa kijamii ambao huhusisha matumizi ya sheria inayoongoza wakati wa kufanya maamuzi ya kiuongozi katika taasisi mbalimbali za kijamii. Vilevile, Ondoro (2021) anafafanua zaidi kuwa siasa inahusisha ushindani baina ya viongozi kwa madhumuni ya kujijengea umaarufu katika jamii. Suala la siasa katika makala hii limechunguzwa hasa katika madaraka ya kiuongozi kupitia wahusika madikteta:

**Wahusika Madikteta**

Kulingana na Liden (2011) udikteta ni hali ya ukiukwaji wa haki za binadamu na uhuru wa mtu mmojammoja. Liden anaeleza kuwa katika utawala wa kidikteta hakuna matumizi ya sheria wala

katiba. Ufafanuzi wa Liden unashabihiana na data ya makala hii kwani, kupitia diwani ya *Wasakatonge* mwandishi ameonesha kuwa suala la uongozi wa kidikteta ni tatizo kubwa katika nchi za dunia ya tatu na hasa Afrika. Hali hii inasababishwa na viongozi wengi wa Afrika kutokuwa tayari kuachia madaraka mara baada ya vipindi vyao vya kiutawala kumalizika. Shairi la "Madikteta" linafafanua jinsi suala la udikteta lilivyo katika nchi za dunia ya tatu kama ifuatavyo:

(4)

**Madikteta,**
Katika,
Dunia hii ya tatu,
Na hasa **Afrika** yetu,
Itele" Mungu" watu"
Bokasa, Idi, Mobutu,
Mizinga nayo mitutu,
Haitoi risasi,
Hutoa maraisi,
Walio **madikteta**.

**Chanzo:** Diwani ya *Wasakatonge* (uk. 21)

Dondoo hii limedhihirisha kuwa katika dunia ya tatu na hasa Afrika suala la siasa linakabiliwa na changamoto ya kukosekana kwa viongozi bora wanaojali maslahi ya wananchi na taifa. Hii ni kwa sababu viongozi wengi wa Afrika hawafuati misingi ya utawala na sheria hali inayowafanya wajione miungu watu. Viongozi hao huongoza kimabavu bila kuzingatia demokrasia. Msingi wa Nadharia ya Uhalisia unaodai kuwa mwandishi huchagua wahusika ambao ni vielelezo na mifano ya watu wanaoishi katika jamii umetuongoza kubaini kuwamwandishi ametumia mfano wa wanasiasa kama Mobutu Rais wa Zaire, Bokasa aliyekuwa kiongozi wa Afrika ya Kati na Idi Amini aliyekuwa Rais wa Uganda, ni dhahiri kuwa wanawasilisha uhalisia uliopo katika nchi za Kiafrika kuwa ni vigumu kusaka demokrasia kwa njia ya mtu mmoja. Hii ni kwa sababu, madikteta huwa na uovu unaotokana na kukumbatia ukabila, udini na hata uvamizi wa nchi nyingine. Vilevile, kukosekana kwa demokrasia katika nchi za Afrika ni suala halisi ambalo limekuwa mwiba mkubwa wa machafuko ya kikabila na kisiasa kutokana na sheria na uhuru wa kuzungumza kukosekana.

**Kigezo cha Kidini**

Dini ni mfumo wa kiitikadi, viashirisho na matendo ambayo hutambulika na kueleweka kwa njia ya imani kuliko njia ya kitaaluma (Malugu, 2016). Naye Marisya (2017) anaenda mbele zaidi kwa kueleza kuwa, dini ni imani inayohusiana na mambo ya kiroho kwamba kuna Mungu ambaye aliumba ulimwengu na ndiye mtawala wa kila kilichomo. Kadhalika, Jesse (2017) anafafanua kuwa dini inamaanisha jumla ya imani ya binadamu pamoja na mafundisho wanayoyatoa kuhusu yale ambayo wanazingatia ama kuyasadiki. Si hivyo tu, bali pia dini inahusu maadili mema na mabaya. Katika utafiti huu tumebaini kuwa mwandishi wa diwani teule ametumia kigezo cha kidini kwa jicho angavu la kumulika uovu unaofanywa na viongozi wa dini. Viongozi hao ni pamoja na Masheikh na Mapadri dhidi ya waumini wao. Hili limedhihirishwa na mwandishi katika diwani ya *Vifaru Weusi* kupitia wahusika Padri na Masheikh:

**Wahusika Masheikh na Padri**

Utafiti huu umebaini kuwa mwandishi ametumia kigezo cha kidini kuwajenga wahusika Masheikh na Mapadri kama viongozi wa dini ya Kiislamu na Kikristo. Katika diwani ya *Vifaru Weusi* imebainika kuwa wahusika Masheikh na Padri ni viongozi wa dini wanaotofautishwa kwa aina ya mavazi yao. Mathalani, Masheikh wao vazi lao kubwa ni juba, aya za kuruani na shanga maalumu zinazotumiwa kuhesabu wakati wa kutaja majina ya mwenyezi Mungu. Kwa upande wa Padri, anatambulika kwa vazi la lenye kola shingoni, msalaba shingoni, biblia mezani na rozari kiganjani. Kadhalika, data ya Makala hii imeonesha kuwa kazi kubwa wanayoifanya ni kuwasifia na kuwatukuza wakuu wa nchi

kwa kupaza sauti katika majukwaa na madhehebuni. Hili limethibitishwa kupitia shairi la 'Mavuvuzela'. Mwandishi anasema:

(5)

**Mavuvuzela**

Mavuvuzela,
Mno mwayapuliza,
Huku mwahanikiza,
Sana yamechagiza,
Masikio kuumiza,
Wengi yamewachukiza,
Wachache kuwapendeza.

Mavuvuzela,
**Masheikh** Jukwaani,
Na majuba mwilini,
Na vilemba
Vichwani,
Tasibihi mikononi,
Kwa aya za kuruani,
Wamsifia mkuu

Mavuvuzela,
**Padri** madhehebuni,
Kafula maungoni,
Msalaba shingoni,
Rozari kiganjani,
Biblia mezani,
Watukuza mkuu.

Mavuvuzela,
Vigogo jukwaani,
Hotuba *mesheheni,*
Ukweli na utani,
Ili wanaamini,
Wawe madarakani,
Wasujudia Mkuu.

**Chanzo:** Diwani ya *Vifaru Weusi* (kur. 54-55)

Katika dondoo hili, tumeona kuwa Masheikh ni watu wanaosimama majukwaani kwa makusudi maalumu yanayosadifu majina yao. Aidha, kulingana na imani yao dhana kama shanga na aya za kuruani zinatarajiwa kutumiwa kwa lengo la kufundisha masuala ya kiroho hususani kwa waumini wao. Kinyume na uhalisia wa nafasi yao ya dini katika jamii, imebainika kuwa wawapo majukwaani kazi yao ni kuwasifia wakuu wa nchi kwa lengo la kuwasaidia waendelee kuwa madarakani. Hali hii inaonesha unafiki wa Masheikh wakijipendekeza kwa viongozi mbalimbali wa nchi kwa kuwasifia viongozi hao badala ya kutekeleza wajibu wao wa kufundisha masuala ya kiroho.

Kwa upande wa mhusika Padri, huyu ni mtumishi wa Mungu na pia kiongozi wa kidini ambaye anatarajiwa kuwa mwadilifu na mnyofu (Mbatiah, 2016). Katika data hapo juu, mhusika padri amesawiriwa katika diwani ya *Vifaru Weusi* akiwa madhehebuni na biblia mezani. Kwa hali halisi kitendo hicho kinaashiria wajibu wake kama kiongozi wa kiroho kutoa mafunzo ya neno la Mungu (Mosha, 2013). Padri ni kiongozi wa kiroho mwenye jukumu la kutoa malezi ya kiroho. Pamoja na ukweli huo, Padri katika utafiti huu, amebainika akitumia biblia kutukuza viongozi wa nchi badala ya

Mungu. Hali hii, imemfanya Padri kuwasujudia viongozi wa nchi kwa sababu ya nafasi na mamlaka waliyonayo na kumsahau Mungu anayestahili kuenziwa.

**Kigezo cha Utaifa**

Kulingana na Miller (1993) utaifa ni kuwa na utambulisho unaodhaniwa kuwaunganisha watu na kuwa jamii moja katika imani, historia, uhusika ulio hai ndani ya mipaka na miiko inayotambulisha kwa jamii nyingine. Katika Makala hii mwandishi wa diwani teule ametumia kigezo cha utaifa kuwaainisha wakazi wa bara la Afrika. Wakazi hao ni Waafrika wenyewe ambao maisha yao yamedokezwa na mwandishi katika diwani zake kama inavyoelezwa hapa chini:

**Waafrika**

Waafrika ni watu ambao waliathiriwa sana na fikra za kikoloni ambazo ziliwafanya waamini kuwa wao ni duni na Wazungu ni bora, wastaarabu na wajuzi wa kila jambo (Msacky, 2015). Hali hii iliwafanya Waafrika kufanya kila kitu na kufikiri kila jambo kwa mtazamo na fikra za Kizungu. Kupitia kigezo cha utaifa Waafrika wamejengwa kama watu duni mbele ya wakoloni, thamani na utu wao ulipotea na kugeuzwa kama wanyama. Katika diwani ya *Vifaru Weusi* shairi la 'Waafrika' mwandishi amelidhihilisha hilo pale anaposema:

(6)

**Waafrika**
**Waafrika**,
Waliwindwa, kama wanyama
Walisagwa, kwa wima wima
Walisombwa, bila huruma
UNYONGE
Ubeberu ulioje!
Wakidi, walichakazwa,
Mijeledi walicharazwa,
Wenye kedi, watelekezwa
UBEBERU
Ukatili ulioje!
Bagamoyo, wanapofika
Sambwe, hukusanyika
Siku hiyo, wakaondoka
UKATITILI
Dhuluma iliyoje!
Zanzibari, wakapelekwa,
Na bandari, kuteremka,
Ni safari, ya kumenyeka,
DHULUMA.

**Chanzo:** Diwani ya *Vifaru Weusi* (kur. 73)

Dondoo hili, limedhihirisha changamoto kadha wa kadha zilizowakabili Waafrika kipindi cha utawala wa Waarabu. Mambo hayo ni pamoja na kuwindwa kama wanyama, kuswagwa wima wima, kusombwa bila huruma, kuchakazwa na kucharazwa mijeledi kwa maslahi ya mabeberu. Aidha, katika makala hii imebainika kuwa Bagamoyo ndiyo kilikuwa kitovu cha biashara ya utumwa, ukatili na dhuluma dhidi ya mwanadamu. Lengo la wakoloni kuendesha dhuluma na ukatili lilikuwa ni kutimiza matakwa yao ya uzalishaji mali katika mashamba yao kwa kuwatumia Waafrika. Suala hili ni kinyume na utu wa binadamu.

**Kigezo cha Kiusimulizi**

Usimulizi katika kazi ya kifasihi hutegemea msimulizi ambaye ndiye ana nafasi muhimu wakati wa kusimulia hadithi au tukio na ni sharti achague njia atakayoitumia kuwasilisha ujumbe (Gennette, 1980). Kadhalika, usimulizi huanishwa kwa kuzingatia nafasi tatu (Stanzel,1984) Ufafanuzi wa

wataalamu hawa unaonesha wazi kuwa mwandishi au mtunzi wa kazi yoyote ile ya fasihi anao uwanja mpana wa kutumia wahusika kulingana na ujumbe unaolengwa kwa hadhira aliyoikusudia. Katika Makala hii imebainika kuwa , mwandishi ametumia kigezo cha usimulizi katika diwani teule kumjenga mhusika nafsi ya kwanza kama alivyochambuliwa hapa chini;

**Mhusika Nafsi ya Kwanza**

Wahusika nafsi ya kwanza ni wahusika ambao usimulizi wao huhusisha matumizi ya nafsi ya kwanza (Stanzel, 1984). Naye, Mohamed (1995) anaeleza kwamba usimulizi wa nafsi ya kwanza huwa si mbinu rahisi kwa mwandishi kwa kuwa viwakilishi vya nafsi havifai kutumika kwa wingi bali kwa umoja tu. Kwa hiyo, uhusika nafsi ya kwanza huweza kuwa bayana kwa kuzingatia viambishi kama vile 'ni' au 'mimi.' Si hivyo tu, bali mhusika nafsi ya kwanza husimulia kuhusu matendo yake mwenyewe na wala si ya wahusika wengine (Wambui, 2018). Katika diwani ya *Wasakatonge* mhusika nafsi ya kwanza amebainishwa kupitia shairi la 'Pepo bila Kifo'. Mwandishi anasema:

(7)

**Pepo bila Kifo**

7 Nataka niifikiye pepo
**Ni**zipate **raha** zilizopo
Na kila kizuri kilichopo
*Nifaidike*

8 **Ni**yanywe maziwa ya uzima,
Na maji baridi ya kisima,
**Ni**uridhiye wangu mtima,
*Niburudike.*

9 **Ni**chote mito yenye asali,
**Ni**yale matunda mbalimbali,
Na vyakula vilivyo anzali,
*Niridhike*

10 **Ni**zitalii bustani zake,
**Ni**one ndege na nyama wake,
**Ni**pumbazwe na maua yake,
*Nifurahike*

11 **Ni**bembee na hurulaini,
Wanawake wazuri wa shani,
Wawashindao wa duniani,
*Nipumbazike.*

12 Pepo ingawa ingali tamu,
Naisubiri kwa nyingi hamu,
Ila kifo ndio kwangu sumu,
*Na siitaki!*

13 Sitaki nilazwe kaburini,
Katika huo mwana wa ndani,
Ubao kuwekwa ubavuni,
*Sitoafiki!*

14 **Si**tataka shida na taabu,
Sitapenda yoyote adhabu,
Bora nikose matulubu
*Nasifariki!*

**Chanzo:** Diwani ya *Wasakatonge* (ukur. 14)

Dondoo hii limeonesha viambishi vinavyowakilisha mhusika nafsi ya kwanza ni **Si na Ni**. Viambishi hivi vimetumika kuonesha adhima na kusudio la mhusika nafsi ya kwanza kutaka kuifikia pepo. Kwa muktadha wa kifasihi peponi ni mahali ambapo hakuna shida zozote zipatikanazo huko na ni mahali ambapo watu huamini kuwa watapata suluhu ya shida wanazokumbana nazo duniani (Musyoki, 2016). Kadhalika, katika shairi la 'Pepo bila Kifo' mhusika nafsi ya kwanza ameonesha peponi ni mahali penye raha, kila kizuri kipo, maziwa ya uzima, maji baridi ya kisima, mito yenye asali, matunda na vyakula vyenye anzali. Pia, peponi kuna bustani nzuri yenye ndege na nyama pamoja na maua. Vilevile, peponi kuna starehe na ili kuzifikia mhusika nafsi ya kwanza (Ni) anaonesha kukwepa kifo na kukiona ni kikwazo kikubwa cha kuifikia pepo. Licha ya njia ya kuifikia pepo kuwa kifo, mhusika nafsi ya kwanza anaona kuwa si lazima kupata shida na tabu ndiyo uifikie pepo na kama ndivyo anaonesha yupo radhi kuikosa., muhimu kwake ni kuwa asifariki. Kupitia kigezo cha usimulizi mhusika nafsi ya kwanza amejengwa kama mtu mnafiki kwani si rahisi kuifikia pepo bila kuingia kaburini.

Vilevile, katika diwani ya *Fungate ya Uhuru* mwandishi ametumia mhusika nafsi ya kwanza katika shairi la 'Nchi Yangu'**.** Kama ilivyoelezwa na Samba (2018) mhusika nafsi ya kwanza ni yule ambaye mwandishi humtumia katika kazi andishi za fasihi kwa mantiki kwamba mwandishi hupotelea ndani ya mmoja wa wahusika wake ambaye husimulia hadithi yote. Samba anadai kuwa katika aina hii ya mhusika, mambo ayasemayo mtunzi huwa yanaelekezewa nafsi moja tu. Mambo hayo yanaweza kuwa maonyo, maelekezo au mawaidha mbalimbali. Hili limebainishwakatika shairi la 'Nchi Yangu'ambapo mwandishi anasema:

(8)

**Nchi Yangu**

Naipenda nchi yangu,
Naipenda, naipenda nitakufa naipenda,
Tailinda nguvu zangu, tailinda,
Tailinda kwa maafa tailinda
Sitakwenda kwa wenzangu,
Sitakwenda kwa wenzangu,
Sitakwenda, sitakwenda hata sifa sitakwenda,
Nitakwenda huku kwangu, nitaganda,
Nitaganda kwa ulofa nitaganda
Nikizipata Bunduki,
Taingia msituni, kuzitumia vitani
Afrika ya Kusini, kumtoa mkoloni
Lovamia, Namibia
Kahamia, Azania
Sauti haiondoshi!

**Chanzo:** Diwani ya *Fungate ya Uhuru* (ukur. 5)

Katika ubeti huu, kiambishi **Ni** kimetumiwa kuwakilisha mhusika nafsi ya kwanza. Aidha, kama ilivyoelezwa na Kemunto (2016) usimulizi wa nafsi ya kwanza huchukuliwa kuwa mmoja kati ya wahusika katika kusimulia hadithi yote. Katika data hiyo, imebaini kuwa masuala mbalimbali yaliyopewa kipaumbele na mhusika nafsi ya kwanza. Mambo hayo ni pamoja na upendo wa dhati juu ya nchi yake, kuwa tayari kutumia nguvu kuilinda nchi dhidi ya maafa. Kadhalika, kigezo cha usimulizi kimetumika kumjenga mhusika nafsi ya kwanza kama mtu mwenye utayari wa kuingia msituni vitani ikiwa atazipata bunduki kwa ajili ya kuifia nchi yake. Lengo la kutaka kuingia vitani msituni ni kumtoa mkoloni. Ili kumuondoa mkoloni suluhu si kuongea tu bali pia utendaji wa vitendo kwa kupambana msituni kwa bunduki ili kuhakikisha amani ya nchi inapatikana. Kwa hiyo, ili nchi iwe na neema na utulivu ni lazima kila mwananchi awe na moyo wa utayari wa kuipambania nchi.

**Kigezo cha Kiishara**

Pauline (2013) anaeleza kuwa mhusika wa kiishara anatumiwa kama muashiriaji katika kazi ya fasihi. Ishara zinazotumiwa katika kazi za fasihi hujengwa na mwandishi kwa kuzingatia muktadha wa jamii na binadamu ndiye hutumia ishara hizo katika mawasiliano (Cameron, 1985). Kadhalika wahusika wa kiishara ni wahusika ambao huwasilishwa kitabia kulingana na majina yao, ambao pia hupatikana katika fasihi simulizi (Saleh, 2015). Tofauti na mtaalamu huyu, Fakih (2017) anaona kuwa wahusika wa kiishara ni wahusika wa kimuundo. Wakati mwingine watunzi hutumia wahusika wa kiishara kuwapa maana fulani ambayo wasomaji wanapaswa waing'amue (John, 2022). Katika diwani teule mwandishi ametumia kigezo cha kiishara kumjenga mhusika mjamzito.

**Mhusika Mjamzito**

Katika diwani ya *Fungate ya Uhuru*, kigezo cha kiishara kimetumika kumjenga mhusika mjamzito kama mtu anayeashiria matatizo ya wananchi yanayotarajiwa kushughulikiwa na viongozi wao wa serikali. Kama ilivyobainika kuwa, njia pekee ya kumrahisishia mwanamke kujifungua ni kupasuliwa kutokana na kushindwa kujifungua kwa njia ya kawaida, ni wazi kuwa hiyo ndiyo njia sahihi ya kuweza kuepuka matatizo yanayowaakumba wajawazito hususan mauti. Suala hili limetazamwa katika shairi la 'Mjamzito'. Mwandishi anasema:

(9)

**Mjamzito**

**Mjamzito** amelazwa thieta!
Lazima kupasuliwa
Chake kitoto, tumboni kinatweta
Hawezi kujifungua
Mwili u moto, Tumbo linamkeketa
Kwa kite anaugua
Jasho na joto, kiungo cha mpwita,
Na mauti yanamwita.

**Chanzo:** Diwani ya *Fungate ya Uhuru* (ukur. 7)

Dondoo hilo linadhihirisha kuwapo kwa changamoto nyingi katika jamii zinazowatazama viongozi wa serikali kama madaktari wanaoweza kuzitatua. Kadhalika, imebainika kuwa suluhu pekee ya kuweza kukabiliana na changamoto hizo ni kufanya upasuaji. Kwa mujibu wa data za Makala hii, upasuaji ni maamuzi ya serikali katika kutatua na ikiwezekana kumaliza kabisa matatizo yanayowakabili wananchi kama vile njaa, elimu na huduma za afya. Katika uhalisia, hii ina maana kuwa si kila tatizo katika jamii linaweza kutatuliwa na wananchi isipokuwa ni lazima maamuzi magumu yachukuliwe na viongozi wa nchi ili kuweza kuwasaidia wananchi wao kuondokana na adha mbalimbali za kimaisha wanazokabiliana nazo.

**Kigezo cha Kifasihi Simulizi**

Ndungo (1991) anaeleza kuwa wahusika wa kifasihi simulizi huweza kuwa watu, wanyama,mazimwi ambao mara nyingine viumbe hao huweza kuwa hata wahusika wakuu. Tofauti na Ndungo, Wamitila (2008) anaona kuwa wahusika wa kifasihi simulizi ni viumbe wasiokuwa na uwezo wa kutenda kama binadamu lakini hupewa sifa za kutenda kama binadamu. Licha ya kwamba wahusika wa kifasihi simulizi wamekuwa wakitumiwa sana katika kazi za fasihi simulizi hususani ngano ni tofauti katika ushairi wa Kiswahili kwani ahusika wa kifasihi simulizi hutumiwa katika mandhari tofautitofauti. Kwa mfano, katika diwani ya *Wasakatonge* mwandishi ametumia wahusika wanyama mbalimbali katika mandhari ya mbugani. Hili limedhihirishwa na mwandishi katika shairi la 'Miamba' kama ifuatavyo:

(10)

**Miamba**

1 Miamba,
**Chui** na **Simba**,
Mbugani wanatamba,
Vinyama vinayumba,
Chakula cha wakubwa,
*Ni sheria za Mbuga?*

2 Waovu,
**Nyati** na **ndovu**,
Mbugani waonevu,
Majani hayaliki,
Ni mboga ya wakubwa!
*Ni sheria za Mbuga?*

3 Vituko,
**Mamba** na **Boko**.
Huleta machafuko
Mtoni masumbuko,
Maji yao makubwa!
Ni sheria za mbuga?

4 Wanyonge,
Wamo shidani,
**Digidigi** na **nyani**,
Wamo makimbizoni
Fisi wanafurahani!
Sheria za mbuga?

**Chanzo:** Diwani ya *Wasakatonge* (uk. 29)

Katika ubeti huu, Khatib ametaja wahusika tofautitofauti wa kifasihi simulizi. Wahusika hao ni pamoja na Simba, chui, mamba, kiboko, digidigi na nyani. Kigezo cha kifasihi simulizi kimetumiwa na mwandishi kuwajenga wahusika kama vile simba, chui na mamba kama tabaka linalojishughulisha na unyonyaji dhidi ya tabaka tawaliwa. Simba, chui, mamba na boko ni wanyama wenye nguvu na mabavu mbugani na majini. Kwa hiyo, mwandishi amewatumia kuwasilisha tabaka la juu la viongozi wanaoongoza nchi kwa mabavu huku tabaka tawaliwa likinyonywa na kunyanyasika. Nyani na digidigi wametumiwa kuonesha tabaka la watu wa chini walio katika shida na tabu zinazosababishwa na sheria mbovu zilizotungwa katika nchi. Kwa hiyo, kutumia wahusika wanyama na mbuga kumesaidia kuonesha hali halisi ya matabaka mawili yaani tabaka tawala na tabaka tawaliwa wanavyoishi chini ya sheria kandamizi inayowabeba watawala na kuwaumiza wataliwa.

Pia, katika diwani ya *Fungate ya Uhuru* mwandishi Khatib ametumia kigezo cha kifasihi simulizi kuwajenga wahusika wa kifasihi simulizi. Mathalani, katika shairi la 'Kunguru' mwandishi amemtumia mhusika kunguru kuwasilisha viongozi walioteuliwa na kuaminiwa kuwa wangekuwa suluhu ya matatizo mbalimbali yanayoikabili jamii. Kinyume cha kuondoa matatizo katika jamii viongozi hao wakageuka kuwa chanzo cha ongezeko la matatizo katika jamii. Mawazo ya Mkonda (2015) yanashadidia kwa kufafanua kuwa kunguru ni ndege mwenye tabia ya wizi na mjanja asiye mwepesi kukamatika. Hili limethibitishwa katika shairi la 'Kunguru'. Mwandishi anasema:

**(11)** **Kunguru**
Kunguru walisafirishwa,
Nchini wakahaulishwa,
Na kazi ikatayarishwa,
Ili **uchafu** kuondoshwa

Kunguru wakabadilika,
**Uchafu** wao wakaweka,
**Maradhi** yakaongezeka,
Ni badala ya kutoweka,

**Wizi** wanauendeleza,
Na **uchafu** kuuendeleza,
Na wenyeji kuambukiza,
**Maradhi** kuyatapakaza,

Kunguru nao wao wenyeji,
Wa mashambani na wa miji,
Wauzidisha **unyonyaji,**
Na maradhi yao ulaji.

**Chanzo:** Diwani ya *Fungate ya Uhuru* (uk. 25)

Shairi hili linaeleza juu ya hatua zilizochukuliwa kukabiliana na tatizo la uchafu nchini. Aidha, tumebaini kuwa Kunguru ndiye mhusika pekee wa kifasihi simulizi aliyekidhi kigezo cha kuweza kukabiliana na tatizo la uchafu katika nchi. Kinyume na matarajio ya nchi, mhusika Kunguru alibadilika na kugeuka kuwa chanzo cha uchafu kilichosababisha kuongezeka kwa maradhi. Makala hii imebaini kwamba uchafu ni matatizo yasiyofaa katika nchi kama vile wizi na unyonyaji. Vilevile, katika nchi nyingi inaaminika kuwa matatizo kama wizi na unyonyaji yanaweza kutatuliwa na watu kutoka nje ya nchi zao. Hata hivyo, imebainika kuwa hali huwa tofauti na matarajio ya wengi kwani mhusika Kunguru aligeuka na kuwa chanzo cha maradhi kutapakaa. Si hivyo tu, bali pia kigezo cha kifasihi simulizi kimewajenga wahusika kunguru kama viongozi waliozidisha unyonyaji mashambani na vijijini. Kwa hiyo, mitazamo na imani ya kuamini kuwa watu kutoka nje ndiyo wanaweza kutusaidia kutatua matatizo yetu si sawa, kwani wao pia hitaji lao kubwa ni ulaji na siyo utatuzi wa matatizo yaliyopo katika nchi.

Kwa upande wa diwani ya *Vifaru Weusi*, Khatib ametumia wahusika wanyama katika kuelezea suala la ubabe unaofanywa na viongozi waliopo madarakani katika bara la Afrika. Aidha, wahusika wanyama ni wahusika muhimu sana katika ulimwengu wa fasihi simulizi (Alhabib na Maguo, 2020). Katika makala hii, imebainikakuwa umuhimu wa wahusika wanyama umejidhihirisha katika kuibua na kuonesha utendaji mbovu wa viongozi katika bara la Afrika. Katika shairi la 'Nyati' mwandishi anasema:

(12) **Nyati**
Katika mbuga Afrika,
Wanyama huwa na hulka,
Wengi wanakarambuka,
Zao kucha na **pembe**
Hukata kama wembe,
Hawakamatiki.

**Ukubwa wao wa umbo**,
**Nguvu zao** na matambo,
Hawayumbi kwa vikumbo,
Ni wanyama wa **kutisha**,
Waweza wakakufisha,
**Hawasogeleki.**

**Chanzo:** Diwani ya *Vifaru Weusi* (kur. 50-51)

Katika shairi hili, mnyama anayetajwa ni Nyati ambaye amejengwa kama mhusika katika mbuga anayetumia pembe kama silaha ya kujilinda. Si hivyo tu, bali pia ukubwa wao wa umbo, nguvu na matambo vinawafanya nyati kuwa wanyama wa kutisha kiasi cha kuwafanya wasisogelewe kirahisi. Aidha, ni wazi kuwa mbuga imechorwa kitaswira. Taswira ni picha wanayoipata wasomaji wa kazi ya fasihi pale wanaposoma kazi fulani ya kifasihi (Hassan, 2013). Kwa hiyo, taswira ya mbuga inawakilisha nchi, na nyati ni viongozi wanaotawala na kuongoza nchi kimabavu. Hii ina maana kwamba suala la demokrasia katika nchi nyingi za Afrika bado ni changamoto ambayo haijapatiwa ufumbuzi. Hivyo, kukosekana kwa demokrasia kumeendelea kutengeneza daraja kubwa kati ya watawala na watawaliwa kiasi cha watawala kushindwa kusogelewa.

**Hitimisho**

Makala hii imejadili vigezo vilivyotumiwa na mwandishi Seif Khatib kuwajenga wahusika katika diwani teule za utafiti huu. Imebainika kuwa vigezo vinavyotumika kuwajenga wahusika katika ushairi wa Kiswahili ni pamoja na kigezo cha kitaswira, kigezo cha uhalisia, kigezo cha kisiasa, kigezo cha kidini, kigezo cha kifasihi simulizi na kigezo cha usimulizi. Matokeo yanaonesha kuwa ukibaini vigezo vilivyotumiwa na mwandishi Seif Khatib katika diwani teule za utafiti huu kuwajenga wahusika ndipo na aina ya wahusika waliotumiwa na mwandishi katika diwani teule wanaweza kubainishwa. Wahusika hao ni pamoja na wahusika halisi, wahusika wa kitaswira, wahusika wa kisiasa, wahusika wa kiishara, na wahusika wa kidini pamoja na wahusika wa kifasihi simulizi. Makala hii imeongeza maarifa katika ushairi wa Kiswahili kwa kutambulisha vigezo vinavyotumiwa kuwatambulisha wahusika katika ushairi andishi wa Kiswahili tofauti na mitazamo inayodai kuwa ushairi andishi wa Kiswahili hauna wahusika bali hutumia wahusika wa ushairi simulizi.

**Marejeleo**


Alhabib, A. na Maguo, O. M. (2020). "Mtindo na Wahusika katika Diwani za Dhifa na Wasakatonge." *Mulika*, 39: kur. 50-65.

Bosibori, B. T. (2016). Mwingilianomatini kati ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali na Mstahiki Meya. Tasinifu ya Uzanili, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Cameron, D. (1985) *Feminism and Linguistic Theory*. London: Macmillan.

Dargan, E. P. (2013). *Studies in Balzac's Realism*. Chicago: Literary Licensing, LLC

Fakih, S. J. (2017). Kutathmini Mabadiliko ya Usawiri wa Mwanamke katika Riwaya ya Utengano na Kamwe si Mbali tena: Utafiti Linganishi. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Gouldin, G. (1961) *Realism*. Richmond: University of Richmond.

Hassan, A. M. A. (2013). *Kuchunguza Vipengele vya Fani katika Mashairi ya Kiswahili: Ulinganishi na Ulinganuzi wa Mashairi ya Euphrase Kezilahabi*. Tasinifu ya M.A Kiswahili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Hussein, E.N. (1988) *Kwenye Ukingo wa Thimu*. Nairobi: Oxford University Press.

John, B. (2005). *The Sea*. London: Picador Print.

Kemunto, N. R. (2016). Mtindo katika Utenzi wa Katirifu. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Khatib, M.S. (1988). *Fungate ya Uhuru*. Dar es Salaam: Macmillan Aidan Limited.

Khatib, M.S. (2016). *Vifaru Weusi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Limited.

Khatib M.S. (2003). *Wasakatonge*. Nairobi: Oxford University Press (T) Limited.

King'ei, K. na Kemoli, A. (2001). *Taaluma ya Ushairi*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Mbatiah, M. (2016) "Wahusika wa Kitashititi katika Gamba la Nyoka." *Kiswahili*, 79: 46-56.

Marques, P. G. (2009). A Brief Intellectual History of Early Realism in IR: A Critical Realism. Paper Presented at the international Association of Critical Realism, Rio de Janeiro july 2009.

Marisya, P. (2017). Mchango wa Sajiili ya Kidini katika Kufanikisha Riwaya Mbili za Ken Walibora Kidagaa Kimemwozea na Ndoto ya Almasi. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Malugu, A. (2016). "Nafasi ya Fasihi katika Kusawiri Suala la Dini". Jarida La Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, 79: 66-77.

Miller, D. (1993). "In Defence Nationality." *Journal of Applied Philosophy*, 10 (1): 3-16.

Mkonda, J. J. (2015). Taswira katika *Fungate ya Uhuru na Wasakatonge*. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dodoma.

Mlacha, (1985). "Wahusika katika Riwaya za Kiswahili Tanzania 1970-1982." *Mulika* 17.

Msacky, E. Y. (2015). *Kuchunguza Dhamira za Kijamii na Kisiasa katika Riwaya ya Siri za Maisha*. Tasinifu ya M.A Kiswahili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mohamed, S. A. (1995). *Kunga za Ushairi wa Kiswahili, Tamthiliya, Riwaya na Hadithi Fupi*. Nairobi: East African Educational Publishers Limited.

Mosha, P. G. (2013). Usawiri wa Mhusika Padri katika Riwaya za Kezilahabi. Uchunguzi katika Rosa Mistika, Gamba la Nyoka na Nagona. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Musyoki, C. N. (2016). Maudhui ya Ubaguzi katika Mhanga Nafsi Yangu. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.

M'Ngaruthi, T. K. (2019). "Umbuji wa Wahusika katika Ushairi wa Kiswahili. Mifano kutoka kwa Diwani ya Jicho la Ndani (S.A. Mohamed, 2002)." *Journal of Education, Humanitiesand Literature*, 2 (6). Nairobi: East African Scholars.

Ndungo, C. W. (1992). Wanawake na Mabadiliko ya Kihistoria katika Fasihi ya Kiswahili. Tasnifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Ogutu, H.O. (2021). "Uchunguzi wa Fani za Lugha Zilivyotumika Kuibua Changamoto za Vijana katika Riwaya Teule za Kiswahili." *Edition Consortium Journal of Kiswahili*. 03(1)

Ondoro, J.V. (2021). Maudhui ya Siasa na Athari zake katika Jamii: Mifano kutoka Diwani ya kaza Macho. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Pauline, R. (2013). Uhakiki wa Kimaudhui na Kifani wa Kidagaa Kimemwozea. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Saleh, K. K. (2015). Ufasihi Simulizi katika Riwaya za Shaaban Robert: Mifano kutoka Adili na Nduguze na Wasifu wa Siti Binti Saad. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Samba, M. R. (2018). Uhusika katika Ushairi wa Kiswahili: *Malenga Vumba, Kichomi na Utenzi wa Fumo Liyongo*. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Maseno, Nairobi.

Samwel, M. Seleman, A. na Kabiero, A. (2013) *Ushairi wa Kiswahili, Nadharia, Maendeleo, mwongozo kwa Walimu wa Kiswahili na Diwani ya Mea*. Dar es Salaam: MEVELI Publishers & Method Samwel.

Sengo, T. Y. S. (2009). Sengo na Fasihi za Kiinchi. Dar es Salaam. The Registered Trustee of Al-Amin Education and Research Academy.

Stanzel, F. (1984). *Theory of Narrative*. Cambridge University Press

Wafula, R. M. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: The Jomo Kenyatta

Waititu, F. na Oyugui, L. (2005). *Mwongozo wa Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Sasa Sema Publications.

Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Kiswahili: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publication Ltd.

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi za Fasihi: Misingi na Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide~Muwa.